

Kenya-Kata ya Embu

Taarifa ya Ushauri juu ya Ukulima na Hali ya Hewa


Kutokana na Idara ya Hali ya Hewa ya Kenya

Machi-Aprili-Mei (MAM) 2014


Vipengee Muhimu kuhusu Utabiri wa Hali ya Hewa

Katika Kenya, Miezi ya Machi-Aprili-Mei inajulikana kama msimu wa mvua wa muda mrefu. Kulingana na Idara ya Hali ya Hewa ya Kenya (KMS) mwanzo wa mvua katika kata ya Embu unatabiriwa kuanza katika wiki ya tatu hadi ya nne ya Machi, na hii ni kawaida ikilinganishwa na miaka iliyopita. Mvua inatarajiwa kunyesha mchana wakati wa alasiri, na jioni huenda kukawa na mvua mzito wakati mwingine. Mvua inatarajiwa kukoma kama kawaida kati ya wiki za tatu na nne za mwezi wa Mei. Upeo wa mvua ni katika mwezi wa nne.

Kwa ujumla, sehemu ya Embu inatarajiwa kuwa na mvua nyingi kuliko kawaida. Usambazaji wa mvua katika sehemu mbalimbali unatarajiwa kuwa mzuri ikiwa ni pamoja na mwanzo na mwisho wa kawaida wa mvua. Katika mwezi wa Tatu (Machi), sehemu nyingi za Embu zinatabiriwa kuwa zenye jua na ukavu, na kuimarika kwa mvua katika mwezi wa nne (Aprili) na wa tano (Mei). Mvua kubwa na ngurumo za radi zinatarajiwa hasa katika mwezi wa nne (Aprili).



"Msimu wa Masika"



Mwanzo na mwisho wa kutarajiwa kwa Mvua ya Msimu MAM2014 "Masika"

Ushauri juu ya Ukulima na Hali ya Hewa

Katika kata ya Embu, mvua inatarajiwa kuwa ya kawaida na uwezekano mkubwa wa mvua nyingi zaidi ya kawaida katika miezi ya Aprili, Machi na Mei. Wakulima wanahitaji kuchukua fursa hii ili kuongeza uzalishaji wa mazao yao kwa kutayarisha mashamba yao. Wakulima wanashauriwa kumaliza kupanda kabla ya mwisho wa Machi, yaani kabla ya mwanzo wa mvua. Ni muhimu kutumia mbinu za kuhifadhi udongo. Utayarishaji wa mashamba unahitaji kufanywa kwa wakati unaofaa ili mimea isichelewe kupandwa. Hali ya ukavu inayotarajiwa mwezi wa Machi ni wakati mzuri wa kushughulikia utayarishaji wa mashamba.

Kutumia mbinu za ukulima pamoja na upandaji miti kama vile kupanda miti na ukulima wa mseto unaweza kupunguza mmomonyoko wa udongo na kuongeza ubora wa maji na udongo. Wakulima wanahimizwa wawe na mbinu ya kuondoa maji ili kuzuia uharibifu wa mimea. Uchimbaji wa mitaro ya kuondoa maji haya unaweza kuzuia mafuriko na pia mmomonyoko unaopoteza udongo wa juu wenye rutuba. Kuchanganya mchanga na mbolea ya shamba kunaweza kutayarisha udongo kwa unyonyaji wa maji.

Mvua inayotabiriwa mwezi wa nne inatarajiwa kuwa na matokeo mazuri kwa mimea inayoota. Wakulima wanashauriwa kulima kwa kiwango kidogo ili kuhifadhi unyevu wa udongo (hasa wakati ulio karibu na upandaji). Wakulima wanashauriwa pia wasiweke mbolea na kiuadudu (madawa ya kuulia wadudu) kabla au wakati wa siku za mvua, na pia kupunguza utumiaji wa mbolea za kisinthetiki ili kuzuia uharibifu wa mbegu kwa chumvi. Wakati wa msimu huu, mbinu za kuweka maji ya mvua zinahitaji kutumiwa ili kuhakikisha kwamba kuna maji wakati wa mvua chache.

Ushauri kuhusu mimea maalum

❖ Ushauri kuhusu mahindi

Wakulima wanashauriwa waanze kupanda mahindi kabla ya mwanzo wa mvua katika wiki ya tatu au nne ya Machi. Mahindi yanafaa kupandwa punde tu hali ya udongo na joto lake linapofaa kwani kuchelewesha upandaji kunaweza kusababisha upungufu wa mavuno.

Kwa sababu mahindi yanahitaji unyevu bora zaidi wa udongo wakati wa upandaji, wakulima wanashauriwa kutumia hatua zinazofaa za kuhifadhi udongo. Kuzuia magugu ni muhimu kwa sababu mahindi hushindana na magugu katika wiki nne au sita hivi baada ya kuchipua. Wakulima wanashauriwa kupanda mahindi baada ya kutayarisha kitalu.

Upandaji mahindi kimseto pamoja na maharage na mimea mingine ya jamii-kunde hudhibiti wadudu (viruka majani, mende-jani, kichimba-bua na kadhalika) . Miaka miwili baada ya ugonjwa wa mahindi wa "Lethal Necrosis" kuripotiwa, ugonjwa huu bado unaendelea kusambaa katika maeneo mapya nchini Kenya ambayo hayakuathirika mbeleni. Wakulima wanashauriwa wahakikishe wametumia mbegu za mahindi zilizothibitishwa na wa endeleo kunyunyiza mahindi kwa kutumia via wadudu vinavyofaa ili kuzuia wadudu kwenye mimea inayokua.

❖ Ushauri kuhusu mtama

Mtama unatarajiwa kukua vizuri wakati wa masika. Wakati wa kupanda mtama, wakulima wanashauriwa kuanza utayarishaji wa mashamba kabla ya mvua. Upandaji kavu (yaani upandaji kabla ya mvua) unapendekezwa sana kwa mtama na ni bora wakulima wapande katika wiki za tatu na nne za Machi. Wakulima wanaweza kuanza kupanda mtama katika mwezi wa pili (Februari) kabla ya kupanda mimea mingine. Katika upandaji kavu, kina cha udongo (yaani urefu wa shimo kwenda chini) kinahitajika kuwa sentimeta tano ikilinganishwa na upandaji unyevu (yaani upandaji wakati udongo una maji) ambapo kina kinahitajika kuwa kama sentimita mbili nukta tano (2.5) hadi sentimita nne.

Wakulima wanashauriwa kuweka mbolea vizuri kwa kuchanganya na udongo. Wakulima wanashauriwa pia kupalilia angalau mara mbili wakati wa kukua kwa mimea. Shamba la mtama halifai kuwa na magugu hasa siku za mwanzo za kukua kwa mmea huu. Upandaji mseto wa kuchanganya mtama na nafaka za jamii kunde (kama maharagwe) unapendekezwa ili kuimarisha matumizi mazuri ya shamba na pia rutuba ya udongo.

Katika siku za mvua chache, wakulima wanatarajiwa kumwagilia maji kwa kutumia mbinu za umwagiliaji wa juu au wa chini. Mvua kubwa inayotarajiwa katika mwezi wa nne inatabiriwa kuwa haitaathiri mmea huu sana, kwani mtama hustahimili uwepo wa maji mengi vizuri sana. Hata hivyo, ili kudumisha rutuba ya udongo, wakulima wanashauriwa kuwa na mfumo wa mifereji.

❖ Ushauri kuhusu Maharagwe

Ili kuwa na mazao mazuri ya maharage, umwagiliaji wa maji ni muhimu. Kwa ajili ya mvua ya kawaida au nyingi inayotarajiwa, uhifadhi wa maji ya mvua unahitajika ili maji haya yatumike wakati wa mvua chache. Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu za umwagiliaji wa mifereji ya juu au chini wakati wa ukavu kwa milimita 50 kwa wiki hadi mwisho wa msimu. Kwa kawaida, joto huwa haina athari mbaya kwa maharage, kama kiwango kizuri cha maji kimo mchangani.

Wakulima wanashauriwa kuweka matandazo kwa kutumia majani makavu (ya ngano, mpunga) au nyasi ili kuhifadhi unyevu wa udongo, kuendeleza ukuzaji wa mizizi, na pia kuimarisha ustahimilifu wa buu la nzi wa maharagwe. Ili kupunguza shida za maradhi, nunua mbegu zisizo na maradhi na mimea ya kaltiva isiyo na maradhi, kisha mimea ipandwe mbali mbali ili kuwe na hewa ya kutosha. Upandaji mimea kimseto kwa kuchanganya maharagwe na mahindi na mtama ni wa maana ili kudhibiti wadudu tofauti (viruka majani, mende-jani, kichimba-bua na kadhalika) na pia kuhimiza utumiaji bora wa shamba.

❖ Ushauri kuhusu mimea ya kahawa

Katika mwanzo wa mvua ya masika, mimea mingi ya kahawa katika eneo la Embu inatarajiwa kuwa na maua. Kahawa hukua vizuri katika udongo usio na maji na ulio na hewa ya kutosha. Kwa sababu ya uwezekano wa mvua nyingi kuliko kawaida (wakati mwingine mvua kubwa) katika Aprili na Mei, wakulima wanashauriwa kuhakikisha udongo unahifadhi tu maji ya kutosha, kwa kina cha mita moja nukta tano (1.5) na mita tatu katika sehemu kavu. Miti ya kahawa hukua vizuri ikiwa pamoja na miti ya kivuli. Wakulima wanashauriwa kupanda mimea pamoja na miti ili kukuipa mimea yao kivuli.

Wakulima pia wanashauriwa kuweka matandazo. Matandazo yana manufaa kadha kwa mimea ya kahawa, kwa mfano, uhifadhi wa unyevu wa udongo wakati wa kiangazi, kuzuia magugu, kuongeza rutuba, na pia kuboresha umbo na uwezo wa udongo kupenya maji. Matandazo pia huimarisha kukua kwa mizizi kwenye mchanga wa juu wenye rutuba ili kuongeza mavuno.

❖ Ushauri kuhusu mimea ya chai

Mimea ya chai hukua vizuri kwenye maeneo yaliyo na mvua wa kutosha na pia asidi kwenye udongo. Kukiwa na mvua inayotarajiwa ya kawaida au inayozidi kidogo, chai hutarajiwa kukua vizuri. Mwanzo wa msimu wa masika ndiyo mwanzo wa majira ya kilele cha mazao ya mimea ya chai. Wakulima wanashauriwa waendeleo na ukataji wa matawi na wachune matawi mawili tu na chipukizi juu ya mimea ili kuendeleza ukuaji katika hatua za kwanza ya ukuaji wa mimea. Wakulima pia wanashauriwa wapalilie mimea yao angalau mara mbili kwenye hatua hii ya kwanza.

Umwagiliaji wa maji kwenye mimea ya chai ni wa muhimu katika kuendeleza mazao bora. Wakulima wanashauriwa kumwagilia maji kwenye mimea wakati wa kiangazi kwa kutumia mbinu za umwagiliaji wa mifereji ya chini au ya juu. Wakulima pia wanaagizwa kuweka mchanganyiko mzuri wa mbolea ndani ya udongo wakati wanapotayarisha shamba. Udongo wabustani ya miche unahitaji kuwa na kipimo cha asidi (yaani pH) cha 5.0 hadi 5.8 (kipimo bora zaidi kikiwa ni 5.6). Udongo huu unahitaji kuondoa maji kwa urahisi, kupukutika kwa urahisi na pia usiwe na maramu, mawe kunikuni au mizizi ya mimea.



BANK-NETHERLANDS
BNPP
PARTNERSHIP PROGRAM

